

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA
SHINYANGA MHE. ZAINAB R.
TELACK KWENYE MAADHIMISHO YA
SIKU YA UHURU WA VYOMBO VYA
HABARI DUNIANI YALIYOFANYIKA
KIMKOA KATIKA UKUMBI WA HOTEL
YA VIGMARK TAREHE 03 MEI, 2017**

*Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,
Kamanda wa Polisi Mkoa,
Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za
Mitaa,
Wakuu wa Taasisi za Umma na Binafsi,
Viongozi wa Dini,
Viongozi wa vyama vya Siasa,
Wadau wote wa Habari,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana,
Habari za Asubuhi!*

Ndugu Waandishi wa Habari,

Awali ya yote, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sisi sote Afya njema na kutufikisha siku ya leo ambayo ni muhimu kwetu sote kuadhimisha siku ya Uhuru wa vyombo vya Habari Duniani.

Kwa namna ya pekee, naushukuru sana uongozi wa “Shinyanga Press Club” kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika siku hii adhimu, najua mngeweza kumualika yeyote kuwa mgeni Rasmi katika maadhimisho haya lakini mkanialika mimi kutokana na upendo na imani kubwa mliyonayo kwangu, nami nawapenda sana na ninaahidi kuendelea kufanya kazi na ninyi nyote.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kama ilivyo kauli mbiu ya maadhimisho ya Uhuru wa Waandishi wa Habari kwa

mwaka huu *“Klabu za waandishi wa Habari zina wajibu wa kuleta amani katika jamii”* Ni ukweli usiopingika kwamba waandishi wa habari mnayo dhamana kubwa sana ya kulinda amani tuliyonayo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mara kwa mara amekuwa akisisitiza kwamba waandishi wa habari ndio nguzo pekee ya kulinda amani ya Nchi hii, amekuwa pia akitoa mifano ya Nchi mbalimbali barani Afrika zilizoingia kwenye vita na machafuko ya wao kwa wao (Civil Wars) kutokana na Kalamu za waandishi wa habari katika Nchi hizo kutumika vibaya.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi hiki ambacho serikali ya awamu ya Tano inatekeleza kwa vitendo uwezeshaji wa ujenzi wa viwanda vidogo na vikubwa, niwaombe sana mtangulize

uzalendo ili Mkoa wetu usonge mbele. Sekta ya Viwanda ni mtambuka ambayo inahitaji pia juhudi zenu za kuandika na kutangaza vivutio vya uwekezaji vilivyopo katika Mkoa wetu.

Ni wajibu wetu sote kama wadau muhimu wa tasnia hii ya habari kuhakikisha kwamba tunafichua maovu ili kulinda amani na utulivu katika Nchi yetu, kwa mfano katika kipindi cha uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, waandishi wa Habari katika Mkoa huu mlifanya kazi nzuri sana kwa kushirikiana vema na serikali hali iliyopelekea uchaguzi kuwa wa amani na utulivu.

Natoa Rai kwenu, kuendelea kufanya kazi kwa weledi lakini pia kwa ubunifu wa hali ya juu pasipo kuvunja sheria za Nchi, ushirikiano wenu na viongozi wa serikali katika ngazi zote uendeleo kuimarika na

pale kunapokuwa na dosari yoyote mnaweza kuwasiliana nasi ili turekebishe na tuweze kuendelea na utaratibu uliopo.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika risala yenu mmesema, sensa ya waandishi wa habari mliyoifanya mwezi Desemba, 2016, Mkoa wa Shinyanga una jumla ya waandishi 90 kati yao waandishi 31 tu ndio wanachama wa “Shinyanga Press Club” binafsi naona waandishi 31 ni wachache sana kwani ni **asilimia 34.4** tu ya waandishi wote 90 waliopo ndio wanachama. Niwaombe Waandishi wote mlioko hapa muwahamasishe waandishi wa habari wenzenu wajiunge na klabu yenu kwa sababu **asilimia 65.6** ya waandishi walioko nje ya klabu ni wengi mnoo kiasi cha kuweza kuwahujumu katika tasnia yenu ya habari. Ni rahisi sana makanjanja wa habari kujipenyeza wakiwa

nje ya mfumo rasmi kuliko ndani ya mfumo.

Mwisho lakini sio katika umuhimu.

Kupitia klabu yenu ya waandishi wa habari mnaweza kubuni vyanzo vya mapato vilivyo halali ili muweze kumudu gharama ndogo ndogo za kuendesha ofisi.

“ Klabu za Waandishi wa habari zina wajibu wa kuleta amani katika Jamii”

“Tuendeleo kulinda amani yetu kwa kuepuka kuandika na kutangaza masuala ya uchochezi”

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kwamba maadhimisho haya ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani, katika Mkoa wa Shinyanga yamefunguliwa rasmi.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.